



Unaweza  
kutuomba kwa  
mkalimani



An Australian Government Initiative

National  
Relay  
Service



Je, wewe ni kiziwi, una ugumu wa kusikia au huongei vizuri?

Piga simu na poka simu kupitia Accesshub.

<https://bit.ly/3KsJfrk>

Teletypewriter (TTY) - 1800 555 630



Sikiliza taarifa hii hapa



## Habari zaidi:

Ofisi ya Kamishna wa Habari ya Victoria  
[ovic.vic.gov.au](http://ovic.vic.gov.au)

Idara ya Afya - Ufaragha  
[health.vic.gov.au/privacy](http://health.vic.gov.au/privacy)

gateway  
health

People living well

### Wangaratta

45-47 Mackay Street,  
Wangaratta, VIC 3677  
Simu: (03) 5723 2000  
Feksi: (03) 5722 2313

### Wodonga

155 High Street,  
Wodonga, VIC 3690  
Simu: (02) 6022 8888  
Simubure: 1800 657 573  
Feksi: (02) 6024 5792

### Myrtleford

32 Smith Street,  
Myrtleford, VIC 3737  
Simu: (03) 5731 3500

Barua pepe: [info@gatewayhealth.org.au](mailto:info@gatewayhealth.org.au)

[gatewayhealth.org.au](http://gatewayhealth.org.au)



Australian Government



VICTORIA  
State  
Government



## Ufaragha Wako



gateway  
health

People living well

# Ufaragha/Usiri Wako

## Je, brosha hii inahusu nini?

Gateway Health itaweka maelezo yako ya kibinafsi kuwa ya faragha. Kuna sheria ambazo zinahakikisha kuwa tunaweka siri maelezo yako.

Brosha hii hueleza kwani Gateway Health inakusanya maelezo yako, ni maelezo gani tunayohifadhi, na jinsi tutakavyotumia, kushiriki na kulinda maelezo yako.

## Kwa nini Gateway Health hukusanya maelezo kuhusu mimi?

Kukusanya maelezo husaidia kujua huduma gani unazozihitaji na kupanga utunzaji bora na wewe.

Si lazima kutuambia maelezo yako yote ya afya lakini itatusaidia kuelewa njia bora ya kufanya kazi nawe na kukusaidia.

## Maelezo gani yanatunzwa kuhusu mimi?

Maelezo yoyote unayokubali kushiriki yanaweza kutunzwa, ikiwa ni pamoja na:

- Jina, anwani, nambari ya simu
- Utaifa na lugha ya kuongea
- Kuwa Aboriginal
- Jina na anwani ya mtunzaji
- Maelezo yaliyopita ya kiafya ikiwa ni pamoja na historia ya matibabu, historia ya matibabu ya familia, na masuala mengine yoyote ya afya
- Habari kuhusu huduma ambazo tumekupa
- Huduma unazopata kutoka mashirika mengine
- Taarifa yoyote ya ziada ambayo unatupa.

## Nani atatumia maelezo yangu?

Watu wanaohusika katika utunzaji na matibabu yako pekee ndio watatumia maelezo yako. Wakati mwingine huduma zingine zinaweza kukusaidia. Tutashiriki tu maelezo yako na huduma zingine ikiwa unakubali.

Maelezo yako yatatumiwa pia na Gateway Health kuboresha huduma zetu, kutusaidia kupanga kwa huduma mpya, kutoa taarifa kwa wanaotufadhili na kukidhi mahitaji yetu ya kisheria. Hii haitajumuisha habari yoyote inayokutambulisha. Watu ambao wanaona maelezo hayo hawatajua kuwa imetoka kwako.

## Je, ninaweza kuangalia rekodi yangu?

Unaweza kuomba kwa kisheria kuona rekodi zako za afya kwa mujibu wa:

- Sheria ya Uhuru wa Habari 1982 (Vic)
- Sheria ya Rekodi za Afya 2001 (Vic)

Ikiwa ungetaka kufikia rekodi zako za kiafya tafadhali wasiliana na:

Afisa wa Rekodi za Wateja  
155 High Street  
Wodonga, Vic 3690  
Simu: (02) 6022 8883

## Idhini ya kushiriki maelezo ni nini?

Maelezo yako yanaweza tu kutolewa kwa huduma zingine ikiwa utatuambia hii ni sawa. Hii inaitwa idhini.

Tunakuomba kuweka saina kwenye fomu ya idhini wakati unapojiandikisha kwa huduma za Gateway Health. Unaweza kutuuliza tusiwape wengine habari zako.

## Je, Gateway Health inalindaje maelezo yangu?

Tunakusanya na kuhifadhi maelezo yako ya afya katika faili salama ya kielektroniki ili tuweze kukutunza kwa njia bora zaidi.

Wafanyakazi, wanafunzi na watu wa kujitolea wote wa Gateway Health wana sheria kali za kufuata ili kuweka maelezo yako kuwa ya faragha.

Wakati fulani Gateway Health inatakiwa kwa kisheria kushiriki habari kuhusu wewe. Hii inajumuisha:

- Kesi za hatua za kisheria chini ya amri ya korti
- Kuripoti magonjwa yanayolazimu kujulishwa
- Uchunguzi wa unyanyasaji au kupuuza wa watoto
- Ukatili wa familia
- Hali ambapo mteja yuko katika hatari ya kujiumiza mwenyewe au mtu mwingine
- Nyakati ambapo hali inamaanisha mteja hawezi kufanya maamuzi

## Je, ninawezaje kutoa malalamiko kuhusu faragha?

Ikiwa unataka kutoa malalamiko tafadhali zungumza na mfanyakazi au jaza fomu ya maoni inayopatikana mtandaoni kwenye gatewayhealth.org.au/contactus/ feedback na katika mapokezi katika ofisi zetu zote.

Au unaweza kuwasiliana:

- Ofisi ya Kamishna wa Habari ya Australia  
T: oaic.gov.au  
Simu: 1300 363 992
- Kamishna wa Malalamiko ya Afya  
T: hcc.vic.gov.au/public  
Simu: 1300 582 113